**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (MB), KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2017 (THE FINANCE ACT, 2017)**

***(Inatolewa Chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge,toleo la Mwaka 2016)***

---

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, Kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Halima James Mdee (Mb), naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017.

**Mheshimiwa Spika,** kabla sijatoa maoni hayo, naomba kutumia nafasi hii kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kulaani na kukemea kwa nguvu zote tabia mbaya ya ubaguzi wa kisiasa dhidi ya wabunge wa vyama vya Upinzani iliyoanza kuzuka ndani ya Bunge. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilisikitishwa sana na kitendo cha baadhi ya wabunge kuomba mwongozo wa Spika wakilenga kuishawishi Serikali isipeleke mgawo wa fedha zilizotengwa katika bajeti kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika majimbo ya wabunge wa upinzani kwa sababu Kambi ya Upinzani ilipiga kura ya hapana wakati wa kupitisha bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Ieleweke kwamba, Katiba ya nchi yetu inasema kwamba nchi yetu ni ya kidemokrasia na yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa. Na katika misingi ya demokrasia; watu wana uhuru wa kuchagua - kwa maana ya kukubali au kukataa. Hivyo, kuwaadhibu wananchi kwa kuwanyima fedha za miradi ya maendeleo ambazo Serikali hii imezikusanya kutoka kwao kwa sababu tu hawakuchagua Chama fulani katika uchaguzi, ni dhambi kubwa ambayo ni Mwenyezi Mungu peke yake anaweza kusamehe.

**Mheshimiwa Spika,** kauli kama hizi za ubaguzi wa wazi kutokana na itikadi za kisiasa, zinaashiria kwamba tumevimbiwa na amani na utulivu katika nchi yetu – tunu ambazo zimetupatia sifa kubwa duniani kama Taifa. Leo tumeanza kubaguana kwa tofauti zetu za kisiasa, lakini kesho tutaanza kubaguana kwa makabila yetu, na keshokutwa tataanza kubaguana kwa dini zetu na hatimaye tutaingia kwenye machafuko makubwa katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Bunge hili ni chombo kinachoaminiwa sana na wananchi. Na wabunge wanaaminiwa na wanaheshimiwa sana na wananchi. Kwa sababu hiyo, Bunge linapotoa kauli au wabunge wanapotoa kauli huwa wananchi wanaamini na kufanyia kazi. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba; Bunge litoe kauli ya kukanusha masuala yote yaliyojadiliwa Bungeni yenye mrengo wa

ubaguzi wa kisiasa kwamba hayakuwa rasmi na kwa maana hiyo yafutwe katika kumbukumbu rasmi za Bunge ili wananchi wasije wakalichukulia kwamba ni jambo rasmi na kuanza kulitekeleza na kusababisha machafuko katika nchi. Aidha, kwa kuwa Mnadhimu wa Serikali aliomba mwongozo akitaka kutoa ushawishi kwamba wabunge wa upinzani wasiulize maswali kuhusu utekelezaji wa bajeti katika majimbo yao kwa kuwa walipiga kura ya hapana; naye pia awaombe radhi watanzania kwa kuwa watanzania ndio walioamua kuchagua wabunge wa upinzani ili waisimamie Serikali na haki hiyo wanayo kikatiba; na zaidi sana watanzania hao hao waliochagua upinzani ndio hao hao wanaolipa kodi kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo, sasa naomba nianze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Fedha uliowasilishwa na Serikali kwa ajili ya kupitishwa na Bunge kuwa Sheria rasmi ya Fedha kwa mwaka 2017.

**Mheshimiwa Spika,** kama ambayo tulisema kuwa Serikali imeleta Bajeti ya ajabu ambayo haijawahi kutokea katika historia ya Tanzania, maajabu yaleyale yameendelea kujitokeza katika Muswada wa Fedha wa mwaka 2017.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeleta miswada miwili ya fedha jambo ambalo ni la ajabu na halijawahi kutokea. Muswada wa kwanza ni Muswada wa Sheria ya Fedha Namba 3 wa 2017 wa tarehe 2 Juni, 2017, na Muswada wa pili ni

Muswada wa Fedha Namba 1 wa 2017 wa tarehe 20 Juni, 2017

**Mheshimiwa Spika,** Tofauti na Muswada wa kwanza, wa tarehe 2 Juni, 2017 ambao ulisomwa kwa mara ya kwanza hapa Bungeni tarehe 14 Juni, 2017 na kupelekwa kwenye Kamati ya Bajeti kwa ajili kufanyiwa uchambuzi; Muswada wa pili wa tarehe 20 Juni, 2017 umeletwa jana tarehe 21 Juni,2017 ukiwa na marekebisho ya sheria mpya sita ambazo hazikuwemo kwenye muswada wa awali, jambo ambalo halikutoa nafasi kwa Kamati na wadau kupitia sheria hizi mpya habla hazijaletwa Bungeni kama inavyoelezwa katika Kanuni ya 84 (3) na (4) ya Kanuni za kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kama serikali ingelikuwa inazingatia Kanuni ilitakiwa kuleta Sheria hizo mpya za kufanyia marekebisho katika Muswada kwa kufuata taratibu Za Kikanuni kama inavyoelekezwa katika kanuni ya 87 (1) ambayo inaelekeza kuwa Muswada unatakiwa kwanza usomwe Bungeni kwa mara ya pili na hapo ndipo serikali inaweza kuleta jambo jipya. Kiliochofanywa na Serikali ni kuwasilisha Muswada mpya wenye namba mpya, tarehe mpya ya kuchwapwa kwenye gazeti la Serikali na pia ambao haujasomwa kwa mara ya kwanza Bungeni.

Kanuni 87(1)hiyo inasema, naomba kunukuu "**Endapo Muswada ulikwishasomwa mara ya pili na haukuwa na mabadiliko, lakini kuna jambo au suala jipya limetokea na**

**linahitaji kuzingatiwa, Mtoa hoja anaweza kumwomba Spika wakati wowote kabla Muswada haujapelekwa kwenye Kamati ya Bunge zima kwamba, Muswada huo urejeshwe tena kwenye Kamati inayohusika**"

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapata tabu sana kuelewa maana ya udharura huu. Dharura hii tena kwa masuala nyeti namna hii yanayohusu fedha za umma, inatia shaka kwamba pengine kuna jambo linalofichwa na njia pekee ya kulificha jambo hilo ni kuwashtukiza Waheshimiwa Wabunge kwa kuleta mapendekezo mapya katika dakika za mwisho kinyume na Kanuni zetu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada ulioletwa leo, kwanza haukufuata utaratibu wa kibunge kwa maana ya kusomwa kwa mara ya kwanza na kupelekwa kwenye Kamati kwa ajili ya kupata maoni ya Kamati ya Bajeti, lakini pili hata haukuletwa kwa hati ya dharura kama ilivyo desturi kwa miswada inayohitajika kupitishwa kwa dharura. Aidha, Serikali haijaoundoa Muswada wa awali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kifupi, muswada huu haujasomwa kwa mara ya kwanza Bungeni jambo ambalo ni kinyume na Kanuni ya 83(1) ya Kanuni za Bunge ambayo inasema kwamba ***"Muswada wowote wa Sheria ambao umetangazwa kwenye Gazeti, unaweza kuwasilishwa Bungeni kufuatana na Orodha ya Shughuli ili kusomwa kwa***

***mara ya kwanza na katika hatua hiyo Katibu atasoma jina refu la Muswada wa Sheria unaohusika bila hoja yoyote kutolewa kwa ajili hiyo".***

**Mheshimiwa Spika,** baada ya muswada kusomwa kwa mara ya kwanza; Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Bunge inaelekeza kwamba, "Spika atapeleka Muswada huo kwenye Kamati inayohusika na Kamati hiyo itaanza kuujadili Muswada huo mapema iwezekanavyo. Inawezekana kabisa kwamba Kamati inayohusika imepelekewa Muswada huu; lakini Kanuni ya 84(2) inaielekeza Kamati iliyopelekewa Muswada huo, kutoa matangazo au barua za mialiko kwa wadau ili watoe maoni yao mbele ya kamati kwa lengo la kuisaidia Kamati kuchambua muswada huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mashaka kama Muswada ulioletwa leo umekidhi masharti ya Kanuni ya 84 (2). Kutokana na ukiukwaji wa Kanuni uliofanyika katika uwasilishwaji wa Muswada huu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba Muswada huu umeletwa kienyeji, na kwa maana hiyo, unakosa sifa za kujadiliwa na kupitishwa na bunge lako tukufu.

## 2. MFUMO WA KODI NA USTAWI WA BIASHARA NCHINI

**Mheshimiwa Spika,** mfumo wa kodi wa nchi yetu kwa mujibu wa taarifa ya **"Tanzania Economic Updates, issue no.7 ya Julay 2015"** ni mfumo mbaya sana ambao kwa upande mmoja kodi zake ziko juu sana na hivyo

kuwakatisha tamaa walipa kodi au kwa maneno mengine unasababisha wafanyabiashara watafute mbinu za kukwepa kodi. Kwa upande mwingi mfumo wetu wa kodi una udhaifu katika makusanyo pale ambapo kodi stahiki inatakiwa kukusanywa. Sasa hivi ndio hali imekuwa mbaya baada ya kuundwa kwa kikosi kazi cha kukusanya kodi na hivyo ku***-by pass*** mfumo wetu wa TRA, jambo ambalo linatengeneza mazingira wezeshi kwa watu kutoa rushwa. Hiki ni kikosi hatari sana katika mfumo mzima wa kukusanya kodi.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na mapungufu hayo pia mfumo wetu wa kodi hauna uhalisia wa kodi inayotakiwa kulipwa pamoja na hali halisi ya uchumi wa Tanzania ambayo ni nchi ya uchumi wa chini **"low income economy".** Taarifa hiyo hiyo inaonesha kuwa, kwa utafiti wa Afrobarometer ni kwamba asilimia 72 ya Watanzania wa kawaida wanashindwa kuelewa ni aina gani ya kodi na tozo wanatakiwa kulipa, kwani makato wanayokatwa wanashindwa kufahamu yanahusisha mambo gani hasa, kutokana na wingi wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaliona jambo hili ni hatari sana kwa mlipa kodi, kwani mlipa kodi akishaanza kuona kwamba hatendewi haki katika mfumo mzima wa kupia kodi kwa kulinganisha na aina ya biashara zake, basi inamlazimu mhusika aanze kutafuta njia mbadala ya kuokoa biashara yake isifilisike kwa kulipa kodi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya 'Doing Business' ya mwaka 2015, inaonesha kuwa kati ya nchi 189 Tanzania inashika namba ya 148 katika vigezo ya urahisi wa ulipaji wa kodi. Wafanyabiashara wa Tanzania wanakabiliwa na wastani wa kodi 49 tofauti tofauti kwa mwaka. Hiki ni kiwango kikubwa kwa nchi za Afrika- Kusini mwa Jangwa la Sahara ambazo kiwango chake ni kodi 38 kwa mwaka. Aidha taarifa hiyo inaonesha walipa kodi wanatumia muda wa masaa 181 kila mwaka katika mchakato wa ulipaji wa kodi. Kamba Rasmi ya Upinzani inaona jambo hili bado ni tatizo katika kuongeza mapato yatokanayo na kodi[1].

**Mheshimiwa Spika,** kuna wataalam wengine wanatoa hoja kwamba, "***The exclusive focus on administrative means does not mean of increasing the collection of Taxes***". Msemo huo tunaweza kuuona kuwa ni kweli kwa maana kwamba wingi wa kodi na viwango vya kodi vilivyopo ndilo vinapelekea watu wengi kukwepa au biashara kufungwa hilo ni tatizo pia, hivyo kuweka mifumo mizuri ya teknolojia ya mawasiliano (IT) katika ukusanyaji bado haitoweza kuongeza mapato yatokanayo na kodi.

**Mheshimiwa Spika,** ugatuaji wa masuala ya kodi kama ambavyo sheria zetu zilizopo zinavyosema ilikuwa ni mfumo

[1] The World Bank Group Macroeconomics and Fiscal Management Global Practice Africa Region

wa kuhamasisha ulipaji wa kodi  na tozo mbalimbali kwa wananchi, kwani kufanya hivyo wananchi wanakuwa na imani kuwa kodi wanazolipa zinawaletea maendeleo moja kwa moja katika maeneo husika. Kitendo cha Serikali kuzinyang'anya halmashauri baadhi ya vyanzo vya mapato vya kwa muktadha huo ni kuwaondolea imani watanzania katika ulipaji wa kodi.

## 3. ADHABU ZA MAKOSA YA BARABARANI NI CHANZO CHA MAPATO?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepokea malalamiko kutoka kwa wananchi hasa wamiliki wa binafsi wa magari na madereva wanaoendesha magari ya usafiri wa umma na biashara zingine kuhusu utozaji wa faini zinazotokana na adhabu za makosa ya barabarani unaofanywa na askari wa usalama barabarani.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha kumekuwa na tabia ya Jeshi la Polisi kutoa taarifa kwa umma kuhusu kiasi ambacho kimekusanywa kwa muda Fulani kutokana na adhabu zinazotokana na makosa ya barabarani. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa adhabu ya kulipa faini inatakiwa kuwa funzo kwa mkosaji na si chanzo cha mapato ya serikali. Kwa sasa imefikia hatua watu binafsi wanaona karaha kumiliki magari na wengine wamefikia hatua ya kuacha kutumia magari kutokana na kero za askari wa usalama barabarani.

**Mheshimiwa Spika**, zipo taarifa zisizo rasmi kuwa imefikia hatua askari wa usalama barabarani kupangiwa idadi ya makosa ambayo wanatakiwa kuwasilisha faini kila siku ambapo ikitokea askari hajafikia lengo basi haruhusiwi kwenda kushiriki mafunzo au kupanda cheo. Suala hili si la kupuuzia hata kidogo, kwa sababu tunajenga taifa la kubambikia wananchi makosa ya barabarani kwa ajili ya kukusanya mapato na pia kushindwa kutoa funzo kwa madereva kwa makosa ambayo yanatosha tu askari kutoa elimu kwa Dereva kwa kosa la kwanza.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na nia njema ya kupunguza ajali za barabarani, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutoa ufafanuzi wa jambo hili ndani ya Bunge lako tukufu kuhusu malalamiko haya au Waziri wa Fedha alete marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani ili Bunge na wananchi wajue kuwa serikali imeweka faini za makosa ya barabarani kama chanzo cha kodi.

## 4. MAPITIO YA MUSWADA WA FEDHA 2017

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa utangulizi huo kuhusiana na mfumo wetu wa kodi, Kambi Rasmi ya Upinzani inapitia muswada ulioletwa wa fedha wa mwaka 2017 kuona ni kwa kiwango gani utaathiri maisha ya walipa kodi wa nchi hii kama ifuatavyo:-

## A. MAREKEBISHO YA SHERIA YA BENKI KUU SURA YA 197 (AMMENDMENT OF THE BANK OF TANZANIA ACT, CAP. 197

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 4 cha muswada kinafanyia marekebisho kifungu cha 32 cha sheria mama kwa kuongeza vifungu vipya vya “3 na 4”. Kifungu cha 3 kinasomeka kama ifuatavyo; ***“All Government and Public authorities shall open and deposit all their moneys with the Bank”.***

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa na maoni tofauti juu ya uamuzi wa Serikali wa kuhamisha fedha zote za taasisi za Serikali kutoka kwenye mabenki ya biashara na kuhamishia Benki Kuu, kwamba uamuzi huu kwani Benki Kuu itakuwa inashindana na mabenki ya Biashara wakati ambapo Benki Kuu inatakiwa kufanya kazi ya uthibiti tu.

Kwa kurejea kauli zilizotolewa na ma-Professor wawili wa uchumi na kunukuliwa katika gazeti la mwananchi la tarehe 13 February 2016 kwamba Serikali iangalie wenzetu wa Botswana na Namibia walifanya nini katika hili, na kama Serikali inataka kuingia katika biashara basi ifunge benki yake ya biashara kama lilivyokuwa lengo la kuanzishwa kwa benki ya NBC na akaunti za taasisi zote za Serikali zihamishiwe huko. Hayo yalisemwa na Prof. Anderson. Wakati huohuo Prof. Gabagambi alihoji kuwa inakuwaje Serikali inahamisha fedha zake wakati huo huo hurudi tena

benki kukopa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kupitia hati fungani.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hoja hizo ni mtazamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba kifungu hiki cha muswada kinachopendekezwa na Serikali kisikubaliwe na Bunge lako Tukufu. Kwa utaratibu huu unaopendekezwa na Serikali dhana ya ushindani wa kibiashara hautakuwa na maana. Serikali iweke mfumo mzuri wa kudhibiti mashirika yanayotumia vibaya fedha zake zinapowekwa kwenye akaunti za Benki za Biashara na sio kuzilundika fedha BOT ambao hawafanyi biashara.

## B. MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA BIDHAA SURA YA 147

**Mheshimiwa Spika,** sehemu ya pili ya Muswada huu inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya ushuru wa bidhaa, Sura ya 147 ya Sheria za Tanzania kwa kuweka viwango maalum (Specific rates) vya ushuru wa bidhaa vinavyotumika kwenye baadhi ya bidhaa. Inaelezwa kwamba viwango hivi vinarekebishwa kwa mujibu wa sheria hiyo na **'kwa kiwango cha mfumuko wa bei'**

**Mheshimiwa Spika,** mapendekezo hayo, yamepelekea kupandisha kodi kwenye bidhaa ambazo uzalishaji wake hutumia malighafi inayozalishwa ndani ya nchi kama vile shayiri, na tumbaku jambo ambalo ni dhahiri litapunguza bei za mazao hayo, na hivyo kupunguza kipato cha

wakulima wa mazao hayo. Kwa mfano kwa mwaka huu wa fedha 2017/18 ushuru wa bidhaa kwenye bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini umepanda kutoka shilingi 429 kwa lita hadi shilingi 450 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 21 kwa lita. Hali kadhalika ushuru wa bidhaa kwenye sigara zisizo na kichungi zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75 umepanda kutoka shilingi 11,854 hadi shilingi 12,447 kwa kila sigara elfu moja ikiwa ni ongezeko la shilingi 493 kwa kila sigara elfu moja. Aidha kwa sigara zenye vichungi ushuru umepanda kutoka shilingi 28,024 hadi shilingi 29,425 kwa kila sigara elfu moja, ikiwa ni ongezeko la shilingi 1,401 kwa kila sigara elfu moja

**Mheshimiwa Spika,** wakulima wa shayiri na tumbaku ni kama vile wamekuwa na bahati mbaya miaka yote. Nasema hivi kwa kwa kila mwaka lazima kodi kwenye bia na sigara ipande. Kwa kufanya hivyo, wamiliki wa viwanda vya bia na sigara, ili wamudu kodi hizo na kuweza kupata faida ni lazima wawaminye wakulima wa mazao hayo kwa kutoa bei ndogo.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni mantiki ya kupandisha kodi kwenye bidhaa zinazozalishwa kwa kutumia malighafi inayozalishwa hapa nchini, kwani kwa kufanya hivyo ni kuwadididimiza wazalishaji wa malighafi hiyo, na ni kuua ari ya mapinduzi ya viwanda hapa nchini kwani ili viwanda viwepo na vizalishe lazima kuwe na sekta

ya kilimo iliyoboreshwa, ambapo wakulima wana motisha ya kuzalisha kutokana na bei nzuri za mazao yao.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza pia kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kwa kufuta ada ya mwaka ya leseni ya magari (Annual Motor Vehicle Licence) na badala yake kupandisha ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya petroli, dizeli na taa kwa kiasi cha shilingi 40 kwa kila lita moja ili kufidia upungufu wa mapato ambao ungetokana na kufutwa kwa ada hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilisema wakati wa uwasilishwaji wa bajeti mbadala kwamba; Hii ni bajeti ambayo kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania inawalipisha watanzania maskini wasio na uwezo wa kumiliki magari kodi ya ada ya mwaka ya leseni za magari (Annual Motor Vehicle Licence Fee) kwa kuihamishia kodi hiyo kwenye ushuru wa bidhaa za mafuta ya petrol, dizeli na mafuta ya taa ambapo athari zake ni kupanda kwa gharama za maisha kwa wananchi masikini. Tulieleza kwamba, kupanda kwa bei ya mafuta kutasababisha kupanda kwa nauli katika sekta ya usafirishaji jambo litakalosababisha kupanda kwa bei za vyakula, kupanda kwa bei za kusaga na kukoboa nafaka kwa kutumia mashine zinazotumia petrol au dizeli kwa wananchi waishio vijijini, kupanda bei kwa pembejeo za kilimo, kushindwa kupata nishati ya mwanga kwa wananchi waishio vijijini kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta ya taa nk. Kwa maneno mengine bajeti hii imelenga

kuwabebesha wananchi maskini mzigo wa kodi kwa matumizi ya anasa ya watu wa tabaka la kati na juu wenye uwezo mkubwa kifedha wa kuweza kumiliki magari na vitu vingine vya thamani kubwa.

**Mheshimiwa Spika,** zaidi ya hayo, tulibainisha kwamba, hakuna chombo chochote cha moto cha usafiri wa barabarani kinachotumia mafuta ya taa; iweje mwananchi wa kawaida asiyemiliki gari atozwe ushuru huo kwenye mafuta ya taa?

## C. MAREKEBISHO YA SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA, SURA YA 290

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kwa kukifanyia marekebisho kifungu cha 31A cha sheria hiyo, ili kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya ushuru wa mabango ya matangazo nchi nzima.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haiungi mkono uamuzi wa Serikali Kuu kukusanya ushuru wa mabango nchi nzima kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Sababu kubwa ya kupinga uamuzi huo ni kutokana na ukweli kwamba ushuru wa mabango ni chanzo cha pili cha mapato katika halmashauri zetu, chanzo cha kwanza kikiwa ni kodi ya majengo (property tax)

**Mheshimiwa Spika,** kuzinyang'anya halmashauri zetu vyanzo vyake vya mapato na kuvihamishia Serikali Kuu kunakwenda kinyume kabisa na dhana ya ugatuaji

madaraka katika Serikali za mitaa (D by D) ambayo kwa kipindi kirefu Serikali hii hii ya CCM imekuwa ikipigia upatu. Aidha, kuzinyang'anya Serikali za Mitaa vyanzo vyake vya mapato kutazidhoofisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuwa sasa zitashindwa kujiendesha na hatimaye zitakufa.

**Mheshimiwa Spika,** ukiachilia mbali mapato yatokanayo na ushuru wa mabango ambayo yamechukuliwa na Serikali Kuu, hata hivyo, Serikali Kuu kupitia Waziri wa Fedha, imefuta ushuru wa huduma (Service Levy)kwenye nyumba za kulala wageni; imefuta ada ya vibali vinavyotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mfano vibali vya machinjio, imefuta ada ya vibali vya kusafirishia mifugo na ada ya vibali vya kuanzisha maduka ya dawa; imefuta ada ya makanyagio minadani nk. ambazo zilikuwa ni vyanzo vya mapato kwa halmashauri zetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani haipingi kufutwa kwa ada hizo ambazo zilikuwa ni kero kwa wananchi. Ila haioni mantiki ya kufuta tozo hizo ambazo zilikuwa zinaziwezesha halmashauri kimapato na hapo hapo kuvitaifisha vyanzo vingine vya mapato kama vile ushuru wa mabango na kodi ya majengo na kuziacha Serikali za Mitaa zikiwa hazina chanzo chochote cha mapato.

**Mheshimiwa Spika,** ni muhimu Serikali Kuu ikaelewa kwamba Serikali za Mitaa ni zao la Katiba ya nchi yetu kwa mujibu wa ibara **ya 143 na 145** ya Katiba hiyo, na kwamba uwepo wa Serikali za Mitaa si hisani ya Serikali Kuu. Kwa sababu hiyo, kufanya jambo lolote linalolenga kuzipuuza au

kuzidhoofisha Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zipo kikatiba ni kuivunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 21 cha muswada kinaongeza kifungu kidogo cha "c" kinachofanyia marekebisho kifungu cha 37 cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, ili kuwatambua wafanyabiashara wadogo, wanaofanya biashara katika maeneo ambayo siyo rasmi kama vile mama lishe, wauza mitumba wadogo, wauza mazao ya kilimo wadogo kama mbogamboga, ndizi, na kadhalika kuwapatia vitambulisho maalum vya kazi wanazofanya.

**Mheshimiwa Spika,** ukitazama lengo la marekebisho yanayopendekezwa na Serikali, unaweza kufikiri kwamba Serikali ina nia njema na hawa wafanyabiashara wadogo. Ikumbukwe kwamba wafanyabiashara hawa wamekuwa ndio wahanga (victims) wakubwa wa uonevu mkubwa unaofanywa na Serikali hii ya CCM dhidi yao. Hawa ndio wamekuwa wakifukuzwa kama digidigi katika kila kona ya mji na kupigwa marufuku kuendesha shughuli zao za kujipatia kipato kwa maana kwamba wanachafua mandhari ya miji. Wamekuwa wakitendewa ubaya kana kwamba wao sio raia wa nchi hii.

**Mheshimiwa Spika,** utaratibu huu Serikali inaotaka kuanzisha wa kuwatambua wafanyabiashara wadogo ni kwa lengo la kuwatoza kodi na ushuru tu na si kwa lengo la kuwasaidia kama ambavyo Serikali inavyotaka kuuaminisha umma.

Kama kweli Serikali ilikuwa na nia hiyo, kwa nini haikufanya hivyo kwa miaka 50 iliyopita tangu imekuwepo madarakani?

**Mheshimiwa Spika,** ni aibu kwa Serikali hii kuwageukia wafanyabiashara wadogo ambao ni wanyonge na maskini kwa lengo la kuwatoza kodi wakati imeshindwa kukusanya mapato makubwa katika sekta ya madini. Shilingi trilioni 105, ambazo Serikali imedai imepoteza katika sakata la Makinikia, kwa nini isijikite katika kuzipata hizo kwanza kabla haijaanza kufikiria kodi kwenye vitumbua na maandazi?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishangaa sana Serikali hii kufikiria vyazo dhaifu vya mapato na kuviacha vile vikubwa ambapo kama Serikali itavisimamia vizuri, kusingekuwa na haja ya kuwatoza mama lishe au wauza mbogamboga ushuru wowote.

## D. MAREKEBISHO YA SHERIA YA POSTA NA MAWASILIANO YA KIELEKTORINIKI SURA YA 306. (AMMENDMENT OF THE ELECTRONIC AND POSTAL COMMUNICATIONS ACT, CAP. 306)

**Mheshimiwa Spika,** dhana nzima ya kifungu cha sheria kinachofanyiwa marekebisho wakati Bunge linatunga sheria hiyo ilikuwa ni kuwapa umiliki watanzania katika makampuni yanayomilikiwa na wageni. Kwa dhana hiyo iliyokuwepo ni dhahiri kwamba kifungu cha 7 cha muswada kina kinzana na dhana mama ya uwepo wa kifungu hicho.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inawaomba waheshimiwa wabunge wajiulize ni kwanini hasa kifungu hiki cha muswada kinafuta tafsiri ya maneno ***"local shareholder".*** Bila kufahamu chimbuko lake ni dhahiri sheria hizi tunazozitunga wenzetu watakaokuja watatuona kama vile hatukustahili kuwawakilisha wananchi katika chombo hiki kitukufu.

**Mheshimiwa Spika**, Ni ukweli kwamba kama mazingira ya ufanyaji wa biashara ni mazuri hakuna sababu hata moja ni kwanini hisa za makampuni yanayojisajili katika soko la hisa zisinunulike. Kambi Rasmi ya Upinzani mbali ya sababu hiyo ya kushindwa kununulika kwa hisa na pia pale ambapo wanunuzi watarajiwa wanakuwa na wasiwasi kwamba mahesabu ya utendaji wa kampuni husika yana dalili za udanganyifu.

**Mheshimiwa Spika,** kama vigezo hivyo vikienda sambamba ni dhahiri hata milango ikifunguliwa kwa raia wasio watanzania ununuzi wa asilimia 25 hauwezi kufikiwa. Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuangalia mifumo yake ya ndani ya uthibiti ni kwa kiwango gani ni **"conducive"** kwa wafanyabiashara nchini kufanya biashara. Na hilo ndilo litakuwa suluhisho la tatizo hili na sio kuongeza wigo kwa wageni, kwani kufanya hivyo kunaondoa dhana nzima ya uwepo wa kifungu hicho.

## E. MAPENDEKEZO YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA MADINI, SURA YA 123 YA SHERIA ZA TANZANIA

**Mheshimiwa Spika,** Muswada unapendekeza marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura ya 123 ya Sheria za Tanzania, kwa kuingiza kitu kinachoitwa 'ushuru wa ukaguzi' ('inspection fee'). Ili kuelewa maana ya mapendekezo haya, ni muhimu tufahamu aina na kiwango cha kodi, ushuru, tozo na malipo mengine ambayo makampuni ya madini yanawajibika kulipa sasa kwa mujibu wa Sheria ya Madini.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Sheria ya Madini kama ilivyo sasa, kodi au ushuru au tozo muhimu kuliko zote ni mrahaba (royalty). Hivyo basi, kwa mujibu wa kifungu cha 87(1) cha Sheria hii, mwenye leseni ya kuchimba na/au kuuza madini anawajibika kulipa mrahaba kwa bei ya mauzo (gross value). Viwango vya mrahaba kwa mujibu wa kifungu hicho ni 1% kwa mawe ya thamani (gem); 3% kwa ajili ya madini ya viwandani (industrial minerals), chumvi na madini ya ujenzi kama mchanga, kokoto, mawe n.k.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, mwenye leseni ya kuchimba madini ya vyuma (metallic minerals) kama vile dhahabu, shaba, fedha (silver) na madini ya kundi la platinum (platinum group of minerals), anawajibika kulipa mrahaba wa 4%. Kwa mawe ya vito (gemstones) na almasi pamoja na madini ya urani (uranium), kiwango cha mrahaba ni 5%.

**Mheshimiwa Spika**, tatizo la Sheria za kusimamia rasilimali zetu kurekebishwa ikiwemo Sheria ya Madini limekuwa linapigiwa kelele na Kambi Rasmi ya Upinzani kwa miaka

mingi. Serikali baada ya Taarifa ya Kamati ya pili ya Makinikia (pamoja na mapungufu yake) imeahidi kuwa Sheria na Mikataba yote ya Madini italetwa Bungeni ili iweze kujadiliwa na kufanyiwa marekebisho.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuhoji kama marekebisho haya yanayopendekezwa katika muswada huu ndiyo kero kubwa iliyokuwa inapigiwa kelele na Bunge na serikali kwa muda wote huu?

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo marekebisho haya yaliyoletwa ndani ya Bunge ambayo kimsingi yamelenga kuongeza Asilimia moja ya ushuru wa ukaguzi yanapingana vikali na sheria hiyohiyo ya madini ambayo kimsingi inamlinda mwekezaji kwa kiasi kikubwa mathalani kupitia "Financial stability Clause" kifungu cha 10 ambacho kinazuia ongezeko lolote la kodi ambalo linaweza kuyumbisha Mtaji wa mwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa badala ya kukimbilia kuongeza asilimia moja ya "Inspection" ili iweze kuongeza mapato ya Serikali, Serikali ilete muswada wa kurekebisha Sheria zote zinazosimamia uwekezaji katika sekta ya madini ili yafanyike marekebisho ambayo yatalinufaisha taifa kuliko kufanya marekebisho haya ambayo yanaanza kuleta mgongano wa sheria yenyewe na si kuioanisha.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya marekebisho hayo ya Sheria, Serikali ilete mikataba yote ya sekta ya madini ili ipitiwe upya na Bunge kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

## F. MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA KODI SURA YA 438 {AMMENDMENT OF THE TAX ADMINISTRATION ACT, (CAP.439)}

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 43 cha muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha 76 cha sheria kwa kuweka kifungu kipya 76(4) kinachosomekwa kuwa;

> **"(4) Interest payable under this section or under any tax law shall not be affected or waived for the reason of delay due to court proceedings or any other dispute resolution process"**

**Mheshimiwa Spika,** kifungu hiki kinataka kuingilia uhuru wa Mahakama pale mlalamikaji anapopeleka shauri lake mahakamani. Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kifungu hiki kitawanyima haki wafanyabiashara ambao kwa njia moja au nyingine wanaweza wasitendewe haki na pia kinaondoa nguvu ya mahakama katika kutoa haki, kwa kuzuia jambo linalobishaniwa hadi uamuzi ufikiwe au utolewe. Hii ni kwasababu hakuna mantiki yoyote ya kupeleka shauri Mahakamani endapo mtuhumiwa hajaridhika halafu mtuhumiwa huyo alazimike kulipa faini kabla Mahakama haijadhibitisha kosa lake. Endapo shauri

linaendelea ni vema mtuhumiwa asilipe faini mpaka pale itakapodhibitika kutenda haki. Katiba yetu inatambua kwa uwazi kabisa hakuna chombo chochote kinachoruhusiwa kuingilia uhuru wa Mahakama. Hivyo, Kambi Rasmi inaitaka serikali kubadili kifungu hiki na badala yake kitoe uhuru kwa Mahakama kama Katiba ya nchi inavyotaka.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 44 cha muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha 78 cha sheria, kwa kufuta kifungu cha "3" na kuweka kifungu kipya kinachosomeka kwamba;

> ***"(3) A penalty under this section shall, in case of income tax, apply separately for a failure to file a tax return that is an estimate or provisional amount, and failure to file a tax return incorporating the final amount"***

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inakiona kifungu hiki kuwa kitakuwa ni kikwazo kikubwa kwa wafanyabiashara wadogo ambao wanataka kurasimisha biashara zao, badala ya kufanya hivyo itawabidi waendelee kukaa kwenye sekta isiyo rasmi na Serikali itaendelea kupoteza hata kile kidogo ambacho ingekikusanya. Kwa maana nyingine ni kuwa kifungu hiki sio rafiki katika kuongeza wigo kwa wafanyabishara kurasimisha biashara zao. Tukumbuke kwamba kufanya biashara kwa mazingira ya nchi hii uanza kwa kubahatisha

na pia elimu ya utunzaji wa kumbukumbu za mahesabu ya biashara ni wafanyabishara wachache wenye elimu hiyo.

## G.MAREKEBISHO YA SHERIA YA BANDARI SURA YA 166 (AMMENDMENT OF THE PORTS ACT, CAP.166)

**Mheshimiwa Spika,** ni kweli kwamba tozo kadhaa zinazotozwa katika bandari, mbali ya kodi inayokusanywa na TRA ikiwa ni moja wapo ya vyanzo vya mapato kwa ajili ya uendeshaji wa bandari husika.

***"wharfage" means a charge imposed in respect of all goods and goods in containers that are (i) loaded or unloaded from a vessel at a public port facility; (ii) unloaded overside from vessel to water or loaded from water to vessel, landed from or placed in the water or loaded on or unloaded from a vehicle within the limits of a public port.***

Hivyo basi, kwa kuwa ***"Wharfage charges"*** ni mojawapo ya tozo zinazotozwa katika bandari zetu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kitendo cha TRA kukusanya tozo hizo na kuwekwa Benki Kuu katika akaunti maalum itakayofunguliwa ni kitendo cha kupunguza ufanisi wa bandari, kwani ufanisi wa bandari unategemea kwa kiasi kikubwa ni kwa kiwango gani inavyojitosheleza kimapato.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaona pendekezo hili la Serikali ni kama ***"kifo cha mfa maji haishi***

***kutapatapa”,*** kwa maana kuwa inakataa kusema ukweli kuwa mapato ya kodi yameshuka vibaya sana, kinachofuata ni Serikali kukusanya tozo na vyanzo vingine vinavyopatikana ili kuendelea kuonekana kuwa mapato ya kodi yameongezeka.

## H. MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI ZA MAJENGO YA MAMLAKA ZA MIJI [AMENDMENT OF THE URBAN AUTHORITIES (RATING) ACT]

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inafanyia marekebisho Sheria ya Kodi za Majengo ya Mamlaka za Miji sura 289 ambapo pamoja na mambo mengine inatoza kodi ya majengo, kwa majengo yaliyofanyiwa tathmini na yasiyofanyiwa tathmini kwa kima cha chini cha shilingi 10,000 na majengo ya ghorofa shilingi 50,000.

**Mheshimiwa Spika,** katika kifungu cha 64 cha muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha 3 cha Sheria. Kifungu hicho kinatoa maana ya neno ‘rateable property’ (nyumba zinazotozwa) kikilenga kuwaondoa katika tozo wananchi wanaomiliki nyumba za tope, tembe na nyingine zinazofanana na hizo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwa nyumba hizo zimeondolewa katika tozo lakini pia ni muhimu sana serikali ingefanya makadirio ambayo hayatawaumiza hata wale wasio na kipato lakini wamebahatika kupata misaada ya kujengewa nyumba za tofali. Wapo wananchi wengi

ambao wamejengewa nyumba kwa misaada kutoka kwa ndugu, jamaa, marafiki, mashirika, taasisi za dini, wafadhili n.k kutokana na hali zao za kiuchumi. Kitendo cha kuwajumuisha katika kodi sio jambo zuri kwani linazidisha hali ya umaskini katika kaya hizo. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuangalia namna bora zaidi ya kufanya ukadiriaji kwa kuangalia pia kipato halisi cha kaya hizo badala ya kujikuta ikiwatoza kodi hata wale wenye hali duni sana kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 kifungu cha 38 ilifuta vifungu vya 31A na 31B vya sheria ya fedha ya serikali za mitaa sura namba 290 ambayo ilitoa mamlaka kwa Halmashauri kukusanya kodi ya majengo kwa mwaka 2016/17.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani kueleza kwa kina umuhimu wa kodi hiyo kubaki katika Halmashauri zetu, serikali ilitia pamba masikioni na matokeo yake wakashindwa kukusanya kodi hiyo kwa ukamilifu na kuziacha Halmashauri kukosa mapato.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa kodi hii irudishwe na kukusanywa na Halmashauri zetu ili ziweze kutekeleza miradi ya maendeleo katika ngazi zao na kwa ukweli kwamba ngazi hiyo ya utendaji ndiyo iliyo na taarifa sahihi kuhusu nyumba ambazo zimesamehewa kulipa tozo na nyumba ambazo zinastahili kulipa kodi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa kodi ya majengo kwa maeneo ya vijijini haitakuwa tofauti na kodi ya kichwa ambayo ilifutwa mwishoni mwa miaka ya tisini. Hii ni kwa sababu yapo maeneo ambayo wananchi wanapata misaada kupitia mfuko wa TASAF. Hii haitakuwa na maana kwa sababu serikali itakuwa imetoa mkate kwa mkono mmoja na kuuchukua kwa mkono mwingine. Hivyo utozaji wa kodi hii ya majengo haina tofauti na kodi ya kichwa iliyofutwa miaka hiyo ya tisini.

**Mheshimiwa Spika**, serikali imekuja na majibu kuwa marekebisho katika sehemu hii yanagusa mamlaka za majiji, Manispaa na Miji pekee na sio Vijijini lakini ukisoma Sheria yenyewe inayofanyiwa na marekebisho kifungu cha tafsiri kinagusa Miji na Mamlaka za Wilaya ambayo ipo chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ambayo inaweka utaratibu wa namna Vijiji na Vitongoji vinavyoweza kutangazwa kuwa mamlaka za Miji Midogo, ambapo kimsingi vijiji ni sehemu ya sheria hiyo. Serikali kwa hili imelipotosha Bunge.

## 5. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa mjadala wa bajeti kwa asilimia kubwa ulijikita katika sheria ya usalama wa Barabarani, sura 168. Kwa bahati mbaya sana hadi tunatayarisha maoni haya pamoja na muswada mpya wa fedha ulioletwa hakuna marekebisho ya sheria hiyo. Kambi

Rasmi ya Upinzani inataka kupata ufafanuzi ni kwa namna gani ada ya mwaka ya Leseni ya Magari (**Annual Motor Vehicle Licence fee)** imefutwa? Vinginevyo Kambi Rasmi ya Upinzani inaweza kuamini kwamba Serikali "**imewahadaa watanzania"**.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi inafahamu kuwa ili Serikali iweze kutekeleza wajibu wake kwa jamii ni lazima kodi zilipwe, jambo hili ni lazima lifanyike. Katika kufanya hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa litakuwa ni jambo la muhimu kuhakikisha kuwa viwango vya kodi vinakuwa rafiki na kodi zinakuwa chache kiasi kwamba hakutakuwa na mlipa kodi kujishauri ni jinsi gani atalipa kodi husika.

**Mheshimiwa Spika,** tunafahamu kwamba muswada wa fedha ambao ndio sheria ya fedha ni ridhaa ambayo Serikali inaipata kutoka kwa wananchi kupitia kwa waheshimiwa wabunge kuwa wako tayari kulipa kodi kama ambavyo inapitishwa na Bunge. Kwa muktadha huo kama waheshimiwa wabunge wanatoa ridhaa yao kuwa tozo na shuru mbalimbali ziongezwe, ambazo kwa muktadha wake zitaongeza gharama kwa malighafi zinazotoka kwa wakulima, maana yake ni kudidimiza kilimo ambacho kinatoa ajira kwa watanzania zaidi ya asilimia 75.

**Mheshimiwa Spika,** kuna usemi unaosema kuwa "**boys in the backroom"** ukiwa na maana kuwa kuna kundi la watu wanaofanya maamuzi lakini hawaonekani sehemu yoyote

lakini lakini maamuzi yao yanakuwa athari kwa kundi kubwa la watu.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani imetumia usemi huo kutokana na ukweli kuwa, sisi waheshimiwa ndio tunaotuna sheria kwa mujibu wa sheria, Serikali kazi yake ni kuleta mapendekezo tu. Lakini kwa kuwa kuna ***"boys in the backroom"*** bunge linakuwa ni chombo cha kufuata maelekezo tu. Hii ni hatari sana katika mustakabari wa Tanzania ijayo.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa sasa ni muda mwafaka kwa chombo hiki kikuu cha kutunga sheria kusimamia mamlaka yake ya kikatiba na kisheria. Imebidi kusema haya kwa uchungu mkubwa kwa kuwa waheshimiwa wabunge wamelalamika kuhusiana na kuondoa ongezeko la sh.40 katika lita moja ya mafuta ya taa, lakini serikali inasema kuwa uwiano kati ya mafuta ya taa na diseli ukiwa mkubwa maana yake unaruhusu uchakachuaji wa mafuta ya diseli. Kwa kigezo hiki maana yake ni kwamba wananchi wetu waendelee kuumia ili kuwaridhisha wachache.

**Mheshimiwa Spika**, majibu hayo ya Serikali yanaonesha kuwa bado kuna udhaifu mkubwa kwa upande wa Serikali katika kuzuia udanganyifu unaofanywa na watu wasio na nia njema na uchumi wa nchi yetu. Kwa Waheshimiwa wabunge kukubali hoja hiyo ya uchakachuaji na kuacha maslahi mapana ya wananchi wetu waliyoyaonesha

wakati wakichangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa fedha ni jambo la ajabu kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

……………………………….

**DAVID ERNEST SILINDE (MB)**

**k.n.y MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI-WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

**22.06.2017**